

**Ayala** ni mnyama jamii ya swala, ambaye anapatikana sana maeneo ya nchi za barini, wana pembe ndefu zilizotawanyika kama mashina ya miti (*Tazama picha juu*).

**Paa** ni jamii ya swala wenye mistari meupe, (Maarufu kama Gazelle kwa lugha ya kiingereza). Paa wanapatikana zaidi maeneo ya ukanda wa joto, kama Afrika. (*Tazama picha chini*). Na pia kwenye biblia kuna watu waliitwa Paa.



*Matendo 9:36 “Na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa”.*

Ayala, Paa na Kulungu ni wanyama gani?

Na Kulungu pia ni jamii ya swala, ambao nao pia wanapatikana nchi za ukanda wa baridi kama Ulaya. (*Tazama picha chini*).



Wanyama hawa kwa pamoja tunawasoma wametajwa katika biblia katika kitabu cha Isaya..

1 *Wafalme 4: 22 “Na vyakula vya Sulemani vya siku moja vilikuwa kori therathini za unga wa mzuri, na kori sitini za ngano.*

23 *na ng’ombe kumi walionona, na ng’ombe ishirini za malisho, na kondoo mia, pamoja na ayala, na paa, na kulungu, na kuku walionona”.*

## Sasa kwanini biblia iwataje wanyama hawa?

Kwanza ni wanyama ambao kimwonekano ni wazuri, na wepesi, na pia wana-mbio sana, (*soma Habakuki 3:19, Isaya 35:6, Zaburi 18:33, 2Samweli 22:34, na 2Samweli 2:18*). simba ni rahisi kumkamata punda milia lakini si swala... Sasa katika roho vijana wanafananishwa jamii ya hawa wanyama wa swala. Vijana wana nguvu na pia kimwonekano ni wazuri kuliko wazee, na pia ni wepesi wa kufanya mambo..

Na ndio maana biblia inatoa maonyo haya..

*Wimbo 2: 7 “Nawasihi, enyi binti za Yerusalem, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, Hata yatakapoona vema yenyeewe”.*

Maana yake usiwe mwepesi kuruka huko na huko kama kulungu kuzichochea tamaa za mwili, waasherati wote biblia imesema hawataurithi uzima wa milele.

*2Timotheo 2:22 "Lakini zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi".*

Maran atha.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii **+255693036618 au +255789001312**

---

### **Mada Nyinginezo:**

*Hayawani ni nini katika biblia?*

Ayala, Paa na Kulungu ni wanyama gani?

*Katika biblia Neno “Mshenzi” linatajwa.Kwanini liwekwe?*

*Wibari ni nani?(Mithali 30:26)*

*Nyinyoro ni nini?*

*Ni kwanini mifugo ya Yakobo iliongezeka kwa wingi kiasi kile?*

**Rudi nyumbani**

Ayala, Paa na Kulungu ni wanyama gani?

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)